

**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**

SHULE YA SEKONDARI SHILUSHI,  
S.L.P 200,  
**MAGU**  
TAREHE \_\_\_\_\_

KUMB. NA. SSS/A.1/.....

SIMU - 0768484638

JINA LA MWANAFUNZI .....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SHILUSHI WILAYA YA MAGU  
MKOA WA MWANZA MWAKA 2021.**

**1.0 UTANGULIZI:**

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (1) katika shule hii mwaka 2021.

Shule ya sekondari SHILUSHI iko katika kijiji cha MAHAHA kata ya SHISHANI; umbali wa kilomita 50 Kutoka mji mkuu Halmashauri ya Wilaya ya Magu. Usafiri wa basi kutoka mjini Magu, unapatikana katika kituo cha mabasi cha Magu. Nauli ni Tsh 4000/=

Shule itafunguliwa muhula wa kwanza (1) na kuanza masomo tarehe 11/01/2021. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021; ndani ya siku saba.

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia:**

**2.1 SARE YA SHULE:** (mchoro Umeambatanishwa)

- (a) Sare ya Shule hii ni **Suruali ya Kijivu yeye mifuko mitatu na shati jeupe mikono mifupi kwa wavulana** na sketi **ya kijivu ndefu na blauzi nyeupe mikono mifupi kwa wasichana.** (kila mmoja awe na sare mbili za shule). Viatu vya ngozi jozi mbili (2) vya rangi nyeusi **vinavyofunika miguu na kufungwa kwa gidamu nyeusi, visigino vifupi.** Na visiwe buti kwa wavulana na wasichana. Soksi **nyeupe kwa wasichana na soksi nyeusi kwa wavulana** fupi zenyen urefu kama penseli.
- (b) Rangi ya hijabu ifanane na sare za shule.
- (c) Sweta la kijivu kwa wote. Mkanda mweusi kwa wavulana.
- (d) sare za michezo kwa shule hii ni T – shirt rangi ya blue bahari na tracksuit ya bluu na raba kwa wavulana na wasichana.
- (e) Miche miwili (2) Mchongoma(1) na mwarobaini(1)

**2.2 DAFTARI KUMI** Na Nane (18), kalamu, Dictionary English to English (kamusi ya kiingereza kwa kiingereza), mkebe wa hesabu, na begi la kubebea madaftari.

**2.3 Chakula cha wanafunzi wa kutwa , Nauli ya kwenda Shulen na kurudi nyumbani pamoja na matibabu yatamhusu mzazi au mlezi.**

**2.4 VIFAA VYA USAFI:-**

- 2.4.A** Ndoo moja ya lita kumi
- 2.4.B** Mfagio mmoja wa mti (chelea)

**3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii:**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995.

- 3.1** Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yenyе dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI; yenyejukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo muhimu ya msingi yafuatayo:
- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
  - b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shulen Lazima.
  - c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalizi ya jioni (kujisomea binafsi) ni muhimu na lazima.
  - d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyininge utakazopewa shulen.
  - e) Kufahamu mipaka ya shule kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
  - f) Kutunza usafi binafsi wamwili, mavazi na mazingira ya shule ni lazima.
  - g) Kuva sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
  - h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
  - i) Kutunza mali za umma ni lazima.

**3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule au kusimamishwa masomo:-**

- a) Wizi
- b) Uasherati
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile; uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kuwa mjamzito/ kupata mimba au kusababisha mimba.
- h) Kuoa au kuolewa
- i) Kutoa mimba
- j) Kugoma, kuchocha na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- k) Kukataa au kugomea adhabu kwa makusudi
- l) Kuwa na simu ya mkononi
- m) Kudharau bendera ya taifa, picha ya rais na fedha.

**4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shulen na mwanafunzi atakapo ripoti ni;**

- a) "Medical examination form" ambayo inapaswa iwe imejazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shulen.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo na makosa ya jinai. Utajaza mara utakaporipoti shule.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yalilyotolewa na shule.
- d) **KILA MZAZI AFIKE KURIPOTI AKIWA NA MWANAYE LA SIVYO HATAPOKELEWA SHULENI.**

5.0 Tafadhali soma kwa umakini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.  
Kauli mbiu ya shule hii; "**ELIMU NI AKILI, NIDHAMU NA MAPAMBANO**".

Nakutakia utekelezaji mwema.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

DANIEL M ALICK  
MKUU WA SHULE